

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA

02 JULAI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA – TAREHE 02 JULAI, 2015

I. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

297. MHESHIMIWA MUSTAPHA BOAY AKUNAAY (MBULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Suala la uegeshaji magari mijini ni mambo yanayotawaliwa na Sheria ya Usalama barabarani:-

Je, kwa nini hapa Tanzania baadhi ya Majiji na Manispaa zimebinafsisha wajibu huo.

298. MHESHIMIWA RITTA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kila mwaka Bunge limekuwa likijadili taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na imedhihirisha kuwa kuna upotevu mkubwa wa fedha za Umma kwenye Halmashauri na Manispaa za miji nchini kote:-

- (a) Je, ni watumishi wangapi wamekamatwa na ni hatua gani walizochukuliwa;
- (b) Je, ni fedha kiasi gani zimepotea;
- (c) Je, ni fedha kiasi gani zimerudishwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

299. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Nchi nyingi duniani zina utaratibu wa kutoa vitambulisho vya uraia kwa kuwatambua Wananchi wake ili kuweza kupanga mipango ya maendeleo mbalimbali:-

Je, kwa nini Serikali inasuasua katika kuwawezesha NIDA kukamilisha mpango huo.

WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

300. MHESHIMIWA DKT. AUGUSTINO LYATONGA MREMA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Katika

Jimbo la Vunjo kuna Makampuni mengi ya Simu yaliyowekeza Minara ya Simu katika Vijiji mbalimbali:-

- (a) Je, Minara hiyo iko katika Vijiji gani;
- (b) Je, kuna mikataba kati ya Makampuni hayo ya simu na Vijiji hivyo;
- (c) Je, ni mapato kiasi gani yamepatikana katika Vijiji hivyo kutokana na uwekezaji wa Minara hiyo.

**301.MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Ujenzi wa minara ya simu katika makazi ya Watu unaendelea katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo mbalimbali nchini:-

Je, minara hiyo ina athari gani kwa maisha ya Watu walio karibu na minara hiyo.

II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

**(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima
na kusomwa Mara ya Tatu)**

Muswada wa Sheria ya Kuwalinda watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi wa Mwaka 2015 (*The Whistleblower and Witness Protection Bill, 2015*)

**(Majadiliano yanaendelea katika ngazi ya
Kamati ya Bunge zima)**

Muswada wa Sheria ya Petroli wa Mwaka 2015(*The Petroleum Bill, 2015*).

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi wa Mwaka 2015(*The Oil and Gas Revenue Management Bill, 2015*).

Muswada wa Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Tasnia ya Uchimbaji Tanzania wa Mwaka 2015 [*The Tanzania Extractive Industry (Transparency and Accountability) Bill, 2015*].

DODOMA

DKT. T. D. KASHILILAH

02 JULAI, 2015

KATIBU WA BUNGE